

**UDAHILI KWA MAFUNZO YA UALIMU NGAZI YA ASTASHAHADA NA STASHAHADA KWA CHUO CHA UALIMU
ELIMU MAALUM PATANDI MWAKA WA MASOMO 2018/19**

Chuo cha ualimu elimu maalumu Patandi kupitia Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE) kinapenda kuwafahamisha wahitimu wa kidato cha nne, sita, walimu kazini na umma kwa ujumla kuwa udahili kwa Mafunzo ya Ualimu ngazi ya Astashahada na Stashahada kwa mwaka wa masomo 2018/19 umefunguliwa rasmi kuanzia tarehe 22 Juni 2018 hadi tarehe 8 Septemba 2018. Masomo yanatarajia kuanza tarehe 04 Octoba, 2018 kama ilivyoelekezwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

Kwa waombaji wa programu ya kozi ya ualimu elimu maalumu watatakiwa ama kuomba moja kwa moja Chuoni, ambapo Chuo kitawasajili kupitia 'Institutional Panel' ya chuo au wanaweza kuomba kupitia tovuti ya Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE) (www.nacte.go.tz) kwa kubofya kwenye 'Apply online (SAVS)' kisha kufuata maelekezo.

Pia tunapenda kuwaarifu wahitimu wa kidato cha nne waliochaguliwa moja kwa moja kujiunga na Chuo chetu, wathibitisha kujiunga na Chuo mwaka wa masomo 2018/2019 kupitia tovuti ya Nacte. Utaratibu wa namna ya kuthibitisha unapatika kwenye tovuti ya NACTE. Mwisho wa kuthibitisha ni tarehe 08 Agosti 2018. Mwanafunzi atakayeshindwa kuthibitisha nafasi yake itachukuliwa na wanafunzi wengine.

Fomu ya kujiunga na mafunzo (join instruction) zitapatikana kwenye mtandao wa Chuo na Nacte hivi punde

Zifuatazo ni sifa za kujiunga na Chuo Chetu kama zilivyoanishwa kwenye Kitabu cha Mwongozo wa Udahili (Admission Guidebook) kilichopo kwenye tovuti ya Baraza.

PATANDI TEACHERS COLLEGE - MERU (REG/TLF/063) - Government
Arumeru District Council - Arusha

S/N	Program Name	Admission Requirements	Admission Capacity	Program Duration (Yrs)	Tuition Fees
1.	Astahhada ya Ualimu Elimu Maalum (tarajali)	(a) Ufaulu wa Kidato cha 4 kwa kiwango cha daraja la I-III. (b) Kipaumbele kitatolewa kwa waliofaulu masomo ya Hisabati na Sayansi; na (c) Aliyehitimu Kidato cha 6 ni sifa ya nyongeza.	145	3	Local Fee: TSH. 600,000/=
2.	Astahhada ya Ualimu Elimu Maalum (Walimu Kazini)	Mwalimu kazini aliyepitia mafunzo ya Ualimu daraja la IIIA na uzoefu usiopungua miaka 2.	40	2	Local Fee: TSH. 600,000/=
3.	Stahhada ya Ualimu Elimu Maalum (Walimu Kazini)	Mwalimu kazini aliyepitia mafunzo ya Ualimu Ngazi ya Stahhada na uzoefu usiopungua miaka 2.	40	2	Local Fee: TSH. 600,000/=

4.	Stashahada ya Ualimu Elimu ya Maalum (Historia na Jiografia)	Ufaulu wa Mtihani wa Kidato cha Sita kwa kiwango cha daraja la I-III na alama zisizopungua "Principal Pass" mbili kwa masomo yanayofundishwa Kidato cha I-IV yakiwemo ya Jiografia na Historia	70	3	Local Fee: TSH. 600,000/=
5.	Stashahada ya Ualimu Elimu ya Maalum (Jiografia na Hisabati)	Ufaulu wa Mtihani wa Kidato cha Sita kwa kiwango cha daraja la I-III na alama zisizopungua "Principal Pass" mbili kwa masomo yanayofundishwa Kidato cha I-IV yakiwemo ya Jiografia na Hisabati	70	3	Local Fee: TSH. 600,000/=
6.	Stashahada ya Ualimu Elimu ya Maalum (Kiswahili na Lugha)	Ufaulu wa Mtihani wa Kidato cha Sita kwa kiwango cha daraja la I-III na alama zisizopungua "Principal Pass" mbili kwa masomo yanayofundishwa Kidato cha I-IV yakiwemo ya Kiswahili na Lugha	70	3	Local Fee: TSH. 600,000/=

Imetolewa tarehe 27/06/2018 na

Ofisi ya Mkuu wa Chuo

Chuo cha Ualimu Elimu Maalum Patandi

Kwa taratibu za usajili wasiliana na namba zifuatazo

Msajili 0757 972753 au 0762 800397

Taaluma 0755 640517 au 0755 264770

Ofisi ya Mkuu wa Chuo 0769 977588 au 0784/0767 851061